# Matarajio lukuki!

## Maoni ya wananchi kuhusu sekta ya gesi





## 1. Utangulizi

Tangu kugundulika kwa kiasi kikubwa cha gesi asilia kusini mwa Tanzania, nchi imekuwa ikijiandaa kukuza mapato na ajira kwa wananchi. Wakati huo huo, hofu kuu mbili zimetawala; kwanza: ‘laana ya rasilimali’ (ambapo uchumi wa nchi haukui kuendana na wingi wa rasilimali, na mapato ya nchi hayakuzi vipato vya wananchi au kuondoa umaskini) na pili; kuwepo kwa matarajio yanayozidi hali halisi ya mapato yatakayotokana na rasilimali hizo.

Kiuhalisia, tangu mwaka 2008, bei ya gesi asilia kwenye soko la kimataifa imekuwa ikishuka. Aidha, amana ya gesi ya Tanzania yenye ukubwa wa futi za ujazo trilioni 56 haiwezi kuwapiku wauzaji wakubwa wa gesi (kama vile Australia, Qatar na Urusi). Hata hivyo, wananchi wengi wanayo matumani makubwa sana kwamba gesi hii itawaletea mabadiliko mengi na mazuri sana..

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) – ambalo ni shirika la umma - lilianzishwa mwaka 1969. Lengo lake kuu ni kusimamia nishati za taifa za mafuta na gesi. TPDC, kwa ushirikiano na makampuni ya kigeni ya gesi yenye utaalamu na uwezo wa kifedha lazima wakubaliane utaratibu wa kuchimba gesi hiyo. Cha kuzingatia ni kuwa makampuni haya yanayo motisha ya kiuchumi ya kudai sehemu kubwa ya faida kutokana na uzoefu wa kufanya makubaliano ya aina hii.

Lakini je, wananchi wa kawaida wanaamini nini kinapaswa kufanyika? Na je, wanatategemea matokeo gani hasa? Je, matarajio yana uwiano gani na uhalisia?

Muhtasari huu umeandikwa na Angela Ambroz and Elvis Mushi
Na umeandaliwa na Twaweza East Africa.
Umetolewa Septemba 2015

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Takwimu za muhtasari huu zimetokana na utafiti wa Sauti za Wananchi wa Twaweza. Sauti za Wananchi ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa, unaofanyika mara kwa mara kwa njia ya simu za mkononi Tanzania Bara. Taarifa kuhusu mbinu za utafiti kwa ujumla (ikiwa ni pamoja na jinsi sampuli wakilishi ilivyobakizwa) vinaweza kupatikana kupitia tovuti ya www.twaweza.org/sauti.

Muhtasari huu unajumuisha takwimu kutoka awamu mbili za utafiti wa Sauti za Wananchi zimetumika: takwimu zilizokusanywa kati ya mwezi Oktoba na Desemba 2013 kutoka kwa wahojiwa 1,562 na takwimu zilizokusanywa mwezi Aprili na Mei mwaka huu (2015) kutoka kwa wahojiwa 1,316.

**Seti kamili za takwimu, madodoso, na ramani za kitakwimu zinapatikana hapa www.twaweza.org/sauti.**

Matokeo muhimu ni:
- Wananchi wanahisi kuwa hawana taarifa za kutosha kuhusu uvumbuzi wa gesi. Wananchi nane kati ya kumi wangependa kupata taarifa zaidi kuhusu gesi hii.
- Wananchi hawana taarifa sahihi: zaidi ya nusu wanaamini kwamba "gesi" tayari imeanza kuzalisha pesa. Aidha, mtu mmoja kati ya sita anatarajia kuajiriwa katika sekta ya gesi (jumla ya ajira milioni 4), na wastani wa mapato unaotarajiwa kwa kila mtu ni karibu Sh. 7,500,000 (ukilinganisha na Sh.2,500,000 inayokisiwa na wataalamu).
- Wananchi sita kati ya kumi wanaamini kwamba uvumbuzi wa gesi asilia utaboresha maisha yao. lakini wengi wana wasiwasi kuwa rushwa itatumika kuwanufaisha watumishi wa serikali.


# 2. Mambo tisa kuhusu mtazamo wa wananchi juu ya gesi asilia ya Tanzania

## Jambo la 1: Wananchi wengi wanataka kupata taarifa zaidi

Wahojiwa waliulizwa kama wamewahi kupata taarifa kuhusu ugunduzi wa gesi kusini mwa Tanzania. Kama ilivyokuwa mwaka 2013, mtu moja kati ya wanne alikuwa bado hajasikia- au hakumbuki kusikia kuhusu ugunduzi wa gesi hivi karibuni (takwimu hazijaoneshwa). Asilimia 76 hawajaisikia sera ya gesi asilia na ile ya maudhui ya ndani (takwimu hazijaoneshwa). Asilimia 73 hawajasikia kuhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini Tanzania (TPDC). Ni asilimia 7 tu wanaoijua TPDC na wanaweza kuelezea kazi zake (takwimu hazijaoneshwa).

Asilimia 77 ya wananchi wanaamini kwamba kuna mtu mwenye wajibu wa kuwapatia taarifa zaidi kuhusu gesi asilia (Kielelezo cha 1). Ni asilimia 3 tu ya wananchi wanaoamini kuwa wanazo taarifa za kutosha, ikiwa wananchi wengi wakiomba taarifa zaidi.

**Kielelezo cha 1: Je, unahitaji taarifa zaidi kuhusu ugunduzi wa hivi karibuni gesi?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* Awamu ya 28 (Aprili – Mei 2015)
Majibu ya "Sijui" hayamo kwenye kielelezo hiki.


Watu wengi wanasubiri vyombo vya habari (51%) na serikali (31%) vitoe taarifa zaidi kuhusu gesi.

## Jambo la 2: Watu wengi wanafikiri kuwa gesi (na pesa) tayari vimeanza kupatikana

Asilimia 53 ya wananchi inaamini kuwa gesi tayari imeanza kuzalishwa na kutumika (kielelezo cha 2). Hii ni ishara ya kwamba wananchi hawana taarifa sahihi: Wataalam wanaamini kuwa gesi iliyogunduliwa hivi karibuni haitapatikana kwa mtumiaji mpaka mwaka 2025. Kwa sasa, kuna kitalu kimoja tu ambacho kinazalisha gesi: kitalu cha gesi kisiwani Songo Songo, kinachoendeshwa na kampuni ya SONGAS Ltd, ambacho kinatoa kiasi kidogo cha gesi kwa ajili ya kuzalisha umeme na kwa matumizi ya kibiashara.

Takribani watu sita kati ya kumi wanaamini kuwa Serikali na makampuni ya gesi tayari wanapokea mapato kutokana na gesi (takwimu hazijaoneshwa). Idadi hii imeongezeka kutoka watu watatu kati ya kumi waliodhani makampuni ya gesi tayari yanazalisha mapato mwaka 2013.

**Kielelezo cha 2: Je, gesi imeshaanza kuzalishwa kwa ajili ya matumizi ya mwananchi?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* - Awamu ya 28 (Aprili–Mei 2015)

## Jambo la 3: Watu wengi wanaamini kuwa ugunduzi wa gesi asilia utaboresha maisha yao

Asilimia 59 ya wananchi wanaamini kuwa uvumbuzi wa gesi utaboresha hali yao ya maisha (Kielelezo cha 3). Idadi ya wanachi wenye mtazamo huu imepungua mwaka 2015 ukilinganisha na mwaka 2013, ambapo wananchi wanne kati ya kumi walioamini kuwa ugunduzi wa gesi ungeleta "mafanikio" maishani mwao na katika maisha ya baadaye ya watoto wao[1].

**Kielelezo cha 3: Je, ugunduzi wa gesi utabadili vipi hali yako ya maisha?**




**Source of data:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 28 (Aprili – Mei 2015). Wasiojibu hawakuingizwa kwenye kielezo hiki.

Pia tuliuliza ni kiasi gani cha fedha wananchi wanatarajia kupata ndani ya miaka kumi kama mapato yote ya gesi yatagawanywa kwa usawa kwa Watanzania. Wastani wa kiasi walichotaja ni Sh.7,343,636 (takribani dola 3,500) kwa kila mtu (takwimu hazijaoneshwa). Kiuhalisia, hakuna anayejua ni kiasi gani cha mapato kitapatikana kutokana na gesi. Lakini makisio ya kitaalamu yanataja kiasi cha Sh 2,500,000 (takribani dola 1,125) kwa kila mtu[2]. Maana yake ni kwamba matarajio ya Watanzania yako juu mara tatu zaidi ya makadirio halisi.

Aidha, matarajio ya wananchi yanatofautiana sana; baadhi ya watu wanatarajia mapato madogo wakati wengine wanatarajia mapato makubwa. (Kwa mfano, nusu ya washiriki wetu walitarajia chini ya Sh 200,000 huku nusu nyingine, wakiwa na matumaini ya kupata pesa nyingi zaidi). Tofauti na hayo matarajio ya wananchi yanadhihirisha kuwa wananchi hawana taarifa sahihi.


[1] "Kusimamia maliasili: Wananchi wanasemaje?" Sauti za Wananchi, Muhtasari Na. 11. 2014.

[2] Makisio ya Shirika la fedha Duniani (IMF) ripoti ya nchi Na. 14/121, inapatikana hapa: https://www.imf.org/external/pubs/ft/scr/2014/cr14121.pdf ripoti hiyo inakadiria mapato ya mwaka dola bilioni 5-6 kati ya mwaka 2029 na 2043. Makisio ya idadi ya watu Tanzania kwa miaka hiyo ni takriban watu milioni 80 hadi 115. Ukigawanya idadi ya watu na makisio ya kipato utapata wastani wa mapato kwa mwaka. Ukijumlisha kwa kipindi cha miaka 15 kati ya 2029 na 2043 unapata jumla ya mapato yanayotarajiwa kwa kila mtu.

## Jambo la 4: Watu wengi wanaamini kuwa watumishi wa serikali/umma na matajiri ndio watakaofaidika zaidi na ugunduzi wa gesi

Mojawapo ya athari hasi au "laana ya rasilimali" ni "ukiritimba wa kuhodhi mapato": yaani, pale ambapo rushwa inaruhusu watu wachache kunufaika kimakosa na mapato ya rasilimali zetu - kitu ambacho kimepanua pengo la kipato kati ya matajiri na maskini. Watanzania wanatarajia pia kuwa: watumishi wa umma watafaidika zaidi na mapato ya gesi. Mwaka 2013, ni mtu mmoja kati ya watatu (31%) aliyeamini kuwa Watanzania wote watanufaika kwa usawa, ikilinganishwa na mtu mmoja tu kati ya wanne (22%) wanaoamini hivyo mwaka 2015 (Kielelezo cha 4).

**Kielelezo cha 4: Ni kundi gani unalodhani litanufaika zaidi na ugunduzi wa gesi?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* – Awamu ya 9, 11, na 28
(Oktoba 2013, Desemba 2013, Aprili – Mei 2015)

## Jambo la 5: “Kwanza, tupatieni umeme kabla ya kuiuza gesi nje ya nchi.”

Takribani nusu ya wananchi waliohojiwa wangependa gesi inapaswa itumike kuzalisha umeme utakaosambazwa ndani ya nchi (Kielelezo cha 5). Matumizi mengine ya gesi ni kuiuza nje ya nchi ili kuongeza kipato cha fedha za kigeni. Wananchi wengi hawaoni ulazima wa kuuza gesi ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki (Kielelezo cha 5).

**Kielelezo cha 5: maoni ya wananchi kuhusu matumizi ya gesi**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 28 (Aprili- Mei 2015).

## Jambo la 6: Wananchi wanatarajia ajira zaidi ya milioni nne


Moja ya matarajio makubwa ya wananchi ni kuwa ongezeko la rasilimali litachangia kukuza uchumi, ajira na hata kipato cha fedha. Wananchi walipoulizwa kuhusu matarajio yao kwenye masuala kadhaa yanayohusu ugunduzi wa gesi – unafuu wa bei na fursa za ajira katika sekta ya gesi zilitajwa mara nyingi zaidi. Wananchi sita kati ya kumi wanaamini kwamba serikali itawekeza mapato ya gesi katika kuboresha huduma za umma (Kielelezo cha 6).

Wananchi wawili kati ya kumi wanatarajia kuajiriwa moja kwa moja katika sekta ya gesi, na wanne kati ya kumi wanatarajia watoto wao au wanafamilia wengine watapata kazi katika sekta hiyo (Kielelezo cha 6). Hii ni sawa na ajira zaidi ya milioni 4[3]. Hali halisi duniani ni kwamba sekta ya nishati inayohitaji mtaji mkubwa huzalisha idadi ndogo ya ajira. Nchini Norway kwa mfano sekta ya mafuta na gesi imeajiri watu 240,000[4] tu.

[3] Kwa kuangalia idadi ya watu milioni 45, ambao 55% wana umri zaidi ya miaka 18 (kama walivyo wahojiwa wa Sauti za Wananchi ). Hii inaleta jumla ya watu milioni 24.7. Na kwa mujibu wa takwimu zetu, mtu mmoja kati ya sita - au 17% - anatarajia kuajiriwa moja kwa moja sekta ya gesi: 17% ya milioni 24.7 ni milioni 4

[4] Tovuti ya shirika la Petroli Norway, taarifa hii imechukuliwa tarehe 7 Julai 2015. http://www.norskpetroleum.no/en/economy/employment-petroleum-sector/

**Kielelezo cha 6: Nitakusomea njia ambazo watu wanaweza kufaidika na sekta ya gesi. Kwa kila njia, niambie kama wewe utafaidika nayo au la.**




**Chanzo cha taarifa:** *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 28 (Aprili – Mei 2015).
Majibu ya ''ndiyo'' tu ndiyo yaliyoainishwa.


## Jambo la 7: Uwazi wa mikataba ni muhimu,–na TV/redio ni vyombo vinavyopendelewa zaidi

Asilimia 85 ya Watanzania wangependa uwazi wa mikataba kati ya wawekezaji na Serikali ya Tanzania (takwimu hazijaoneshwa). Sheria mpya ya uwazi na uwajibikaji kwenye sekta ya madini ina kifungu kinachohimiza mikataba ya madini kuwekwa wazi kwa umma.Asilimia 64 ya wananchi wanasema wanadhani "rushwa" ndio chanzo cha mikataba kutokuwa wazi[5] (takwimu hazijaoneshwa). Ni asilimia 15 tu ya wananchi wanaodhani mikataba haiku wazi kwa ajili ya usalama wa taifa (takwimu hazijaoneshwa).

Wananchi sita kati ya kumi (59%) wangependa taarifa hizo zisambazwe kwa njia ya redio, televisheni (luninga) au magazeti (Kielelezo cha 7). Ingawa kuna shauku kubwa juu ya masharti ya mikataba hii, ukweli ni kwamba mara nyingi mikataba inaandikwa kwa lugha ya kitaalamu ambayo wengi wanaweza wasielewe. Vyombo vya habari (au watendaji wengine) wanatakiwa kutafuta njia ya kupanua uelewa wa wananchi wa mikataba hii.

[5] Kumbuka kuwa swali hili lilikuwa wazi kwa majibu mengi; waliohojiwa hawakupewa orodha ya kuchagua, hivyo majibu yalikuwa papo kwa papo.

**Kielelezo cha 7: Ni kwa njia gani taarifa za mikataba zisambazwe kwa wananchi?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi*,- Awamu ya 28 (Aprili – Mei 2015)
Majibu ya"Sijui'', wasiojibu, na "nyingine" (1%) yameondolewa kwenye kielezo hiki. Takwimu kamili zinapatikana hapa www.twaweza.org/sauti.

## Jambo la 8: Mwananchi moja kati ya watano anataka Bunge lisimamie mapato ya rasilimali

Tuliwauliza wananchi, "je, ni taasisi, shirika au idara gani inayopaswa kusimamia mapato ya rasilimali?" Asilimia 27 ya wananchi walisema "hakuna" au "hawajui" (Kielelezo cha 8), lakini Bunge lilionekana kuaminika zaidi. Wananchi wawili kati ya kumi walitaja Bunge kama chombo kinachopaswa kusimamia mapato ya gesi (Kielelezo cha 8). Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kawaida huaminiwa sana na wananchi[6] – alitajwa na wachache sana (asimila 8 tu) katika jambo hili (Kielelezo cha 8). Taasisi zenye wajibu wa kudhibiti ubadhirifu wa mali za umma (kama vile Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, au kamati mbalimbali za usimamizi za Bunge) na TPDC yenyewe, pia zilitajwa na watu wachache (Kielelezo cha 8).

6 Wananchi 71% walisema wanaimani na Rais "sana" au "kwa kiasi fulani" -"Wananchi wanaleta mabadiliko:? Je, wananchi wako tayari kushiriki kuleta mabadiliko kuiwajibisha serikali?" Sauti za Wananchi, Muhtasari Na 15. 2014

**Kielelezo cha 8: Ni chombo gani cha serikali unachokiamini zaidi kusimamia mapato yanayotokana na ugunduzi wa gesi?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 28 (Aprili–Mei 2015)

## Jambo la 9: Watu watatu kati ya wanne hawazijui sera za gesi zinazoandaliwa

Ipo sera ya gesi asilia ya mwaka 2013, na sera ya maudhui ya ndani inaandaliwa. Sera ya maudhui ya ndani inajaribu kuhakikisha kuna angalau kiwango cha chini cha wananchi kuajiriwa, na kiasi muafaka cha huduma au bidhaa za Tanzania kutumika na makampuni ya kigeni. Hata hivyo, wananchi watatu kati ya wanne hawajawahi kuzisikia sera hizi mbili (takwimu hazijaoneshwa).

Suala moja la kuzingatia ni jinsi gani wawekezaji na serikali watagawana faida itokanayo na mauzo ya gesi.Asilimia 55 ya wananchi wanaamini kuwa sehemu kubwa ya faida inatakiwa kwenda serikali ya Tanzania. Asilimia 30 wanaamini faida lazima igawiwe sawasawa (Kielelezo cha 9).

**Kielelezo cha 9: Je, mgao wa kiasi gani wa faida ya gesi utakuwa wa haki kati ya wawekezaji wa kigeni na serikali ya Tanzania?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi* – Awamu ya 28 (Aprili – Mei 2015)
Majibu ya "nyingine", "kakataa kujibu" na "Sijui" hayako kwenye kielezo hiki. Takwimu kamili zinapatikana hapa www.twaweza.org/sauti.

# 3. Hitimisho

Ugunduzi wa gesi ni tukio muhimu sana nchini Tanzania. Taarifa za habari kutoka wa vituo mbali mbali zimetawaliwa na taarifa za ugunduzi wa gesi hii: uwazi wa mikataba au mapato vikiandikwa mara kwa mara kwenye magazeti na kutangazwa redioni. Hata hivyo, wakati wananchi wengi wanafahamu kuhusu maliasili hizi, wachache tu ndio wenye taarifa sahihi kuhusu kiasi halisi cha gesi na faida inayoweza kupatikana.  Kwa mfano, wananchi wengi wanaamini kwamba gesi imeshaanza kuzalishwa kwa wingi na kwamba mapato tayari yanapatikana. Pia wananchi wengi wanatarajia mapato makubwa kutokana na mauzo ya gesi (takribani mara tano zaidi ya pato la taifa kwa kila mtu mmoja), na wanatarajia kupata ajira nyingi katika sekta hiyo. Lakini wananchi wengi (watatu kati ya wanne) hawajawahi kusikia kuhusu sera kuu mbili zinazoandaliwa kwa ajili ya kusimamia baadhi ya masuala muhimu katika sekta hii, kama vile jinsi mapato yatavyogawanywa na jinsi huduma, bidhaa na wafanyakazi wa nchini wanavyoweza kutumiwa na sekta hiyo.

Wananchi hawana taarifa za kutosha kuhusu gesi ikiwa ni asilimia 3 tu wanaosema kuwa wana taarifa za kutosha kuhusu sekta hiyo. Hata hivyo, redio ni chanzo kikuu cha taarifa kwa wengi (70%, takwimu hazijaoneshwa). Asilimia 59 wanataka uwazi wa mikataba baina ya serikali na makampuni ya kigeni.

Wananchi wanadai uwazi na uwajibikaji kwenye maswala ya usimamizi wa rasilimali hii ya gesi asilia. Asilimia 77 ya wananchi wanataka mtu wa kuwapatia taarifa na idadi kubwa zaidi (85%) wanataka taarifa za mikataba kati ya Serikali na makampuni ya gesi ya kigeni yawekwe wazi. Kuhusu mapato, wananchi wamegawanyika. Watatu kati ya kumi hawajui wamuamini nani kusimamia fedhaWachache  wamelitaja Bunge kama chombo kinachofaa kusimamia mapato ya gesi asilia. Inawezekana Bunge limetajwa kutokana na kuibua kashfa nyingi za rushwa na kusisitiza uwajibikaji wa wahusika hivi karibuni.

Ishara kubwa ya laana ya rasilimali hutokea zaidi wakati wananchi hawana taarifa au wana taarifa zisizo sahihi. Matarajio yao hayalingani na hali halisi ya sasa au ya baadaye. Serikali yoyote itakayokuwa madarakani inahitaji kuwa makini, hasa katika kuwapatia wananchi taarifa sahihi, za ukweli na zenye kuaminika. Wakati wa kushughulikia matarajio ya wananchi ni huu. Katika jambo hili, subira haitavuta heri.